JARIDA MAALUM LA

# USHIRIKA

**USHIRIKA HUJENGA KESHO ILIYO BORA KWA WOTE**



# MAADHIMISHO YA USHIRIKA DUNIANI - 2024

# YALIYOMO


- SERIKALI INAUNGA MKONO MAGEUZI NA MATOKEO CHANYA SEKTA YA USHIRIKA......................**03**
- USHIRIKA UTUMIKE KUWAKOMBOA WANANCHI ..........................................................................**06**
- DC TABORA AVITAKA VYAMA VYAUSHIRIKA KUZINGATIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA ..................**07**
- MATUMIZI YA STAKABADHI ZA GHALA YANACHOCHEA USHINDANI WA BEI ZA MAZAO SOKONI......**08**
- BENKI YA TAIFA YA USHIRIKA MBIONI KUZINDULIWA..................................................................**10**
- WANAUSHIRIKA WATAKIWA KUJISAJILI KWENYE MUVU..........................................................**12**
- WANAUSHIRIKA WAHIMIZWA KUTUMIA MIFUMO YA KIDIGITALI KUONGEZA TIJA ...........................**14**
- JUKWAA LA WANAWAKE LA VYAMA VYA USHIRIKA LISAIDIE KUWAINUA WANAWAKE................**16**
- MATUKIO MBALIMBALI YALIYOJIRI WAKATI WA SUD ...................................................................**18**

## SERIKALI INAUNGA MKONO MAGEUZI NA MATOKEO CHANYA SEKTA YA USHIRIKA - NAIBU WAZIRI MKUU




***Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akiongea na Wanaushirika wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD),2024***

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko, amesema Serikali itaendelea kuunga mkono mageuzi chanya yanayofanyika kukuza sekta ya Ushirika.

Ameyasema hayo wakati akifunga Maadhimisho ya Ushirika Duniani Julai 6, 2024 katika Viwanja vya Ipuli, Mjini Tabora.

Amesema miongoni mwa hatua za mageuzi hayo ni pamoja na uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ambayo itamilikiwa na wanaushirika kwa asilimia 51 inayotarajiwa kuzinduliwa karibuni.

Aidha, amepongeza uanzishwaji wa Mfuko wa Tafiti za Ushirika utakaosaidia kuibua changamoto na kuzitafutia suluhu.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amesema tayari Serikali imetoa Shilingi Bil.13 za Ruzuku kwa wakulima wa Tumbaku kwa lengo la kufidia gharama za uzalishaji na amesema kuwa Serikali itaendelea kutoa Ruzuku kwa mazao mengine.

rajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema tayari Tume imeunda na inatumia Mfumo wa TEHAMA wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa sekta ya Ushirika, ambapo vyama 6,319 vimesajiliwa kwenye Mfumo.

**Maadhimisho hayo yamefanyika kuanzia**
29 Juni, 2024 yakiambatana na makongamano pamoja na maonesho ya bidhaa na huduma za Ushirika.

Aidha, Katika Maadhimisho hayo Naibu Waziri Mkuu amezindua Tovuti rasmi ya Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane 2024.



***Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizindua tovuti maalum ya maonyesho ya Kimataifa ya Nanene 2024.***



***Naibu Warajis na Warajis Wasaidizl wakishiriki maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani- 2024.***



*Wananchi wakifuatilia siku ya Ushirika Diniani-2024.*



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Abdulmajid Nsekela.*




*Watumishi wa Tume ya Mendeleo ya Ushrika Tanzania (TCDC) wakishangilia ushindi wa banda bora katika maonyesho ya SUD - 2024.*

# USHIRIKA UTUMIKE KUWAKOMBOA WANANCHI KIUCHUMI- NAIBU WAZIRI



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde (Mb) akiongea na Wanaushirika wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani 2024 katika Viwanja vya Ipuli, Tabora***

Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde (Mb) ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na taasisi nyingine zinazohusika na Ushirika kusimamia vyema uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ili viweze kutumika kama nyenzo ya kuimarisha uchumi na kuondoa umasikini.

Akifungua Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Julai 1, 2024 katika Viwanja vya Ipuli Mkoani Tabora amesema Serikali ina azma ya kuhakikisha inasimamia na kuimarisha Vyama vya Ushirika ili viwasaidie Wananchi wengi kiuchumi kupitia Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), SACCOS na Ushiri- ka wa aina nyingine.

Amesema mifumo ya Ushirika imewezesha bei za mazao mbalimbali kuongezeka, akibainisha mfano bei ya kakao kuongezeka kutoka wastani wa Shilingi 7,000 kwa kilo msimu wa 2022/2023 hadi wastani wa Shilingi 29,000 kwa kilo msimu wa 2023/2024.

Aidha, katika msimu wa 2021/2022 Vyama vya Ushirika vilitumika katika usambazaji wa pembejeo mbalim- bali ili kuweza kuwafikia wakulima wake kwa urahisi zaidi, ambapo Jumla ya Shilingi. 1,172,239,240,501 zilitumika kuagiza Pembejeo za aina mbalimbali ikiwemo mbolea ya Ruzuku.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Tume itaendelea kusimamia Vyama kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu na kuwataka viongozi wa Ushirika kuendesha Vyama kwa Uadilifu na weledi.

Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na Wadau mbalimbali ikiwemo Vyama vya Ushirika, Taasisi za Fedha, Makampuni ya Bima, TEHAMA, watoa huduma pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Maadhimisho hayo yameongozwa kwa Kauli Mbiu isemayo "Ushirika Hujenga Kesho Iliyobora kwa Wote".



***Wananchi mbalimbali wakisiliza Hotuba ya Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde (Mb) wakati wa Maadhimisho ya Ushirika 2024.***



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde (Mb) akitembelea mabanda ya maonyesho wakati wa maadhimisho ya ushirika 2024.***

# DC TABORA AVITAKA VYAMA VYAUSHIRIKA KUZINGATIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA



***Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mhe. Deusdedis Katwale akiongea na wanaushirika wakati wa Kongamano la Mazingira kwenye Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024.***

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mhe. Deusdedis Katwale ameviasa vyama vya ushirika nchini kuzingatia masuala ya utunzaji wa Mazingira katika shughuli zao

Mhe. Katwale ameyasema hayo Julai 02,2024 wakati akifungua Kongamano la Mazingira katika siku ya pili ya maadhimisho ya wiki ya Ushirika kwenye viwanja vya Nanenane Ipuli Mjini Tabora, ambapo ames- ema pamoja na vyama hivyo kuwa vinafanya kazi nzuri ya kuwaunganisha wanachama na kuwakwamua kiuchumi lakini kumekuwa na changamoto ya uharibifu wa mazingira katika baadhi ya shughuli zao za uzaishaji ikiwemo kilimo cha Tumbaku.

“Kwanza niwapongeze wana ushirika kwani mmekuwa mkifanya kazi nzuri sana katika Taifa letu, lakini kuna baadhi yenu mmekuwa mkiharibu mazingira katika shughuli zenu jambo ambalo ni hatari kwa viza- zi vya sasa na vijavyo,” amesema Mkuu wa Wilaya ya Tabora.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi, Naibu Mrajis -Uhamasishaji, Consolata Kiluma amesema Tume ya Maende- leo ya Ushirika inahimiza uhifadhi wa mazingira na imekuwa ikifanya kazi pamoja na wadau mbalimbali. Hivyo, amevitaka vyama vya Ushirika kuendelea na uhifdhi wa mazingira kwa manufaa ya vizazi vy6a sasa na vya baadaye.



***Naibu Mrajis (Uhamasishaji) Consolata,akizungumza wakati wa Kongamano la Mazingira katika Maadhimisho ya Ushirika Duniani- 2024.***



***Wanaushirika na wananchi mbalimbali wakifuatilia majadiliano wakati wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani 2024.***

# MATUMIZI YA STAKABADHI ZA GHALA YANACHOCHEA USHINDANI WA BEI ZA MAZAO SOKONI




***Mkuu wa Wilaya ya Uyui Mhe. Zakaria Mwansasu, akieleza jambo alipotembelea banda la Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala wakati wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024.***

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unachangia kuongeza thamani ya mazao na kuwezesha kupata bei zenye ushindani zinazoleta tija na faida kwa Wakulima na Jamii.

Kauli hiyo imetolewa Julai 4, 2024 na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Mhe. Zakaria Mwansasu, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwenye Siku maalum ya Stakabadhi za Ghala wakati wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani katika Viwanja vya Ipuli, Mjini Tabora.

Mhe. Mwansasu amesema hadi kufikia Machi 2024, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala imeratibu ukusanyaji wa mazao kilogramu milioni 371 yenye thamani ya shilingi Bilioni 905.

Baadhi ya mazao yaliyohusika katika Mfumo huo ni pamoja na Mbaazi kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Manyara ambayo yaliingiza Shilingi Bilioni 1.6 kwa Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato kwa mkulima shilingi Bilioni 94.6; Kakao kwa Mikoa ya Morogoro na Mbeya ambazo yalizipatia Shilingi Bilioni 1.4 Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato kwa mkulima Shilingi Bilioni 102.9 kwa mkulima; Korosho kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma na Morogoro ambayo ilizipatia Shillingi Bilioni 7 kwa Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato kwa mkulima shilingi Bilioni 407.9.

Akiongea katika Kongamano la Stakabadhi ya Ghala, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ya Ghala, Asangye Bangu, amesema Bodi hiyo inaendelea kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kutoa rai ya kuongeza matumizi ya mizani za kidijitali pamoja na matumizi ya TEHAMA.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, ametoa wito kwa Wanaushirika kukusanya mazao yenye ubora ili kuepusha usumbufu kwa wanunuzi na Mfumo mzima wa Stakabadhi ya Ghala.

# MATUKIO MBALIMBALI SIKU YA GHALA



***Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu akielezea mchango wa matumizi ya Stakabadhi za Ghala katika Uchumi kwa Wanaushirika.***



***Mbunge wa Jimbo la Chato na Mjumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza kwenye kongamano la Siku ya Ghala - 2024.***



***Wanaushirika wakifuatilia mada na majadiliano kuhusu Stakabadhi za Ghala.***




***Mkuu wa Wilaya ya Uyui Mhe. Zakaria Mwansasu akipata ufafanuzi katika Madhimisho ya Ushirika - 2024.***

# BENKI YA TAIFA YA USHIRIKA MBIONI KUZINDULIWA




***Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Hussein Omar, akipata maelezo kuhusu Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) kwenye Maadhimisho ya Ushrika - 2024.***

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dkt. Hussein Omar, ametoa wito kwa Wanaushirika kuendelea kuchangia Mtaji wa Uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kununua Hisa za Benki hiyo.

Amesema hayo Julai 3, 2024 wakati wa Siku Maalum wa Benki ya Ushirika katika Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani katika Viwanja vya Ipuli, Mjini Tabora.

Amesema kuwa ni muhimu kwa wanaushirika kuwa na Benki yao ili kuwa sehemu ya maamuzi ya Benki hiyo pamoja na bidhaa za Kifedha za Benki hiyo na kuwa sehemu muhimu ya kuchangia kuwa na Uchumi wa Juu wa kati ifikapo 2050 kupitia Kilimo na Ushirika.

Akizungumza katika Maadhimisho hayo, Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro, Godfrey Ng'urah, amesema tayari hatua muhimu za uanzishaji wa Benki hiyo zimekamilika na sasa ni masuala machache yanatarajia kukamilika hivi karibuni.

Ameongeza kuwa Benki hiyo itakuwa chombo muhimu kwani wanaushirika watakauwa ni sehemu ya kunufaika na Gawio la faida ya Benki.

Benki hiyo ya Taifa ya Ushirika inaundwa na muunganiko wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro pamoja na Benki ya Ushirika ya Tandahimba ambayo inatarajia kuanza hivi karibuni.

# MATUKIO MBALIMBALI SIKU YA BENKI YA USHIRIKA



*Mwenyekiti wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), Prof. Gervas Machimu, akizungumza kwenye Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024.*



*Wanaushirika wakifuatilia mada na majadiliano kuhusu kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania*




*Viongozi mbalimbali wa Sekta ya Ushirika wakiwa katika majadiliano ya uanzishwaji na uendeshaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika.*



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akieleza utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Hussein Omar Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024.*



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Nsekela, akipata maelezo kuhusu maendeleo ya Mfumo wa TEHAMA wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), katika Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024*

# WANAUSHIRIKA WATAKIWA KUJISAJILI KWENYE MUVU

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Nsekela, ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika kujisajili kwenye Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao unasaidia Ushirika kujiendesha kibiashara na kuongeza tija na manufaa kwa wanachama.

Ameyasema hayo alipotembelea banda la Tume wakati wa maadhimisho ya Ushirika Duniani na kupata maelezo ya maendeleo ya Mwenendo wa vyama kujisajili wakati wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani Julai 5, 2024 katika Viwanja vya Ipuli, Tabora.

Aidha, Mwenyekiti ameitaka Tume kuendelea kuusimamia na kuboresha zaidi utendaji wa Mfumo wa MUVU ili uendane na kasi ya maendeleo ya kidijitali na kiteknolojia kwa malengo ya kuhudumia vyema Wanachama na Vyama vya Ushirika utakaowezesha kuchangia utunzaji na upatikanaji wa taarifa za vyama, kuongeza uwazi na ufanisi wa utendaji katika Sekta ya Ushirika.

Katika hatua nyingine kwenye kilele cha maadhimisho hayo Mwenyekiti akiwasilisha hotuba yake kwa wanaushirika amesema Ushirika ni nyenzo inayoweza kutumika kujenga kesho iliyo bora kama kaulimbiu ya Maadhimisho isemavyo "Ushirika hujenga kesho iliyo bora".


Hivyo, ametoa rai kwa Wanaushirika kuutumia Ushirika kujikwamua kiuchumi kwa kuutumia Kibiashara ili kujiongezea kipato na ku- jikomboa kiuchumi kwa kuhakikisha Vyama ambavyo bado havijasajiliwa katika Mfumo huo vijisajili katika Mfumo wa MUVU ili kurahisisha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Ameongeza kuwa miongoni mwa Vipaumbele vya vya Tume ni pamoja na kuhakikisha kuwa Vyama vinaboresha utendaji wake kwa kutumia Mifumo ya Kidijitali jambo ambalo litaongeza ufanisi na kupunguza changamoto za Vyama vya Ushirika.

# MUVU KLINIKI NDANI YA SUD



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde (Mb) akipata maelezo kuhusu Mfumo wa MUVU toka kwa Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Hermis Luragirwa.***








***Timu ya wataalamu wa Mfumo wa MUVU wakishiriki kutoa elimu kuhusu Mfumo huo kwenye Maadhimisho ya Ushirika - 2024.***




***Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushrika na Mtendaji Mkuu wa COPRA, Irene Madeje, akifungua kongamano la Kitaifa la Ushirka - 2024.***

# WANAUSHIRIKA WAHIMIZWA KUTUMIA MIFUMO YA KIDIGITALI KUONGEZA TIJA

Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushirika, Irene Madeje, ametoa wito kwa Wanaushirika na Wadau wa Vyama vya Ushirika kutumia Mifumo ya kidigitali katika uendeshaji, uchakataji wa taarifa pamoja na utunzaji kumbukumbu wa taarifa za Ushirika.

Ametoa kauli hiyo Julai 05, 2024 wakati akifungua Kongamano la Kitaifa la Ushirika kwaniaba ya Mwenyekiti wa Kamisheni, Abdul- majid Nsekela, katika maadhimisho ya Ushirika kwenye Viwanja vya Ipuli, Tabora.

Bi. Madeje amesema matumizi ya Mifumo ya TEHAMA yanaongeza kasi ya utendaji bora na kuongeza ufanisi kutokana na utunzaji sahihi wa taarifa, kuongeza uwazi unaosaidia taarifa kupatikana kwa urahisi kwa ngazi mbalimbali za kiutawala hivyo, kuleta manufaa kwa wanaushirika.

Aidha, ameongeza kuwa matumizi ya Mifumo ya Kidigitali kuongeza tija kupitia Mifumo ya TEHAMA katika Minada ya mauzo ya mazao ya Wakulima kutokana na kuongeza wigo wa wanunuzi wa mazao kutoka maeneo mbalimbali ya uzalishaji na Wakulima wanapata fursa ya kufuatilia mwenendo wa mauzo hayo mahali popote kupitia mtandao.

Kwa upande wake Naibu Mrajis (Uhamasishaji), Consolata Kiluma, amesema Kongamano hilo linajadili namna ambavyo Ushirika una- changia katika kuboresha utendaji na hali ya Ushirika unaogusa maisha na hali za Wanaushirika kwa Maendeleo ya sasa na baadaye.

Awali Wanaushirika walijadili kuhusu Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Ushirika - 2024 ***" Ushirika Hujenga Kesho iliyo Bora kwa Wote".***

***Majadiliano hayo yaliongozwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.***

# UWASILISHAJI NA MAJADILIANO YA MADA MBALIMBALI




*Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu, akiongea na Wanaushirika katika Siku ya Ghala wakati wa Maadhimisho ya Ushirika Duniani - 2024.*



*Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) Charles Jishuli, akieleza umuhimu wa Vyama vya Ushirika katika matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.*



*Wanaushirika na wageni mbalimbali wakifuatilia majadiliano kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.*



***Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda , Biashara, Kilimo na Mifugo, Mhe. Mariam Ditopile, akiongea kwenye Jukwaa la Wanawake Wanaushirika katika Maadhimisho ya Ushirika - 2024.***

# JUKWAA LA WANAWAKE LA VYAMA VYA USHIRIKA LISAIDIE KUWAINUA WANAWAKE

Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda , Biashara, Kilimo na Mifugo, Mhe. Mariam Ditopile, amesema kuanzishwa kwa Jukwaa la Wanawake wa Vyama vya Ushirika Tanzania kiwe ni kichocheo cha ongezeko la idadi ya wanachama wanawake kwenye vyama vya Ushirika.

Mhe. Ditopile amesema hayo Julai 5, 2024 mjini Tabora wakati wa ufunguzi wa Jukwaa hiloambapo amesema ni muhimu kuwekamikakati madhubuti ya uhamasishaji kwani taarifa zinaonesha kuwa bado idadiya wanachama wanawake ni ndogo.

Kwa upande wake, Naibu Mrajis– Uhamasishaji, Consolata Kiluma, amesema lengo la kuanzishwa kwa Jukwaa hilo ni kujadiliana juu ya malengo waliojiwekea katika utekelezaji wa shughuliza kiushirika katika kipindi cha mwaka mzima na kuweka mikakati mipya mahali penye changamoto.






***Wanaushirika wakiwa katika jukwa la wanawake wa vyama vya Ushrika.***

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA JUKWAA LA WANAWAKE




*Viongozi Wanawake wakiwa katika Jukwaa la Wanawake wa Vyama vya Ushirika.*



*Wanawake kutoka kwenye vyama vya Ushirika mbalimbali wakisikiliza hotuba na majadiliano ya Jukwaa la Wanawake.*



*Wanawake wanaushirika wakifurahia Jukwaa la kwanza la Wanawake wa Vyama vya Ushirika.*

# MATUKIO MBALIMBALI YALIYOJIRI WAKATI WA SUD



***Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege akipokea Tuzo kwa kufanikisha Benki ya Taifa ya Ushirika kuandikishwa.***



***Mkuu wa Wilaya ya Gairo Mhe. Jabir Makame, akipokea Tuzo ya Mhamasishaji Bora wa Ushirika.***



*Mwanafunzi wa Elimu ya Msingi akipokea Cheti na zawadi kwa ushindi wa uandishi wa Insha za Ushirika.*



*Mwanafunzi Elimu ya Sekondari akipokea Cheti na zawadi kwa ushindi wa uandishi wa Insha za Ushirika.*

# MATUKIO MBALIMBALI YALIYOJIRI WAKATI WA SUD



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege akiangalia Samaki wakavu katika Banda la Ushirika la Mkoa wa Mwanza wakati wa Maadhimisho ya SUD - 2024.*




*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, akitembelea mabanda ya maonessho wakati wa Maadhimisho ya Ushika - 2024.*




*Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro, Godfrey Ng'urah (kulia) akifafanua jambo sambamba na Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika TACOBA, Yahya Kiyabo (kushoto) katika mfululizo wa mahojiano ya Vipindi vya "Tuongee Asubuhi" cha Star TV wakati wa Maadhimisho ya Ushirika - 2024.*



*Wananchi wakipata maelezo na huduma za afya wakati wa Maadhimisho ya SUD - 2024.*




*Naibu Warajis na Warajis  Wasidizi wa Mikoa wakiwa katika Picha ya Pamoja na Mgeni rasmi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati) wakati wa Maadhimisho ya Ushirika -  2024.*




*Baadhi ya watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakiwa kwenye Picha ya Pamoja katika banda la TCDC kwenye Maadhimisho ya Ushirika - 2024.*




**_Watumishi wa TCDC wakitoa huduma mbalimbali za Ushirika wakati wa Maadhimisho ya Ushirika - 2024._**






**_Msanii Mrisho Mpoto akitoa burudani ya nyimbo na ngoma katika Maadhimisho ya Ushirika - 2024._**

# USHIRIKA

Pamoja Tujenge Uchumi

## MAKAO MAKUU YA TUME

Mtaa wa Kuu, S.L.P 201 Dodoma
+255 026 - 2322456
+255 026 - 2321973
ushirika@ushirika.go.tz
www.ushirika.go.tz
ushirika_tcdc
Tume ya Maedeleo ya ushirika